

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 36 **JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC)** FEBRUARI 2024

SHULE YA SEKONDARI YENYE MIUNDOMBINU YA KISASA KUZINDULIWA HIVI KARIBUNI



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania

[tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)

TUNAWAPA KONGOLE WALIMU KWA ONGEZEKO LA UFAULU WA WANAFUNZI

Hivi karibuni Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) lilitangaza matokeo ya mtihani ya Kidato cha Nne uliofanyika Novemba 2023 ambayo yameonesha ufaulu umeongezeka kwa asilimia 0.87 ikilinganishwa na mwaka 2022.

Katibu Mtendaji wa NECTA, Dkt. Said Mohamed alisema jumla ya watahiniwa 572,359 walisajiliwa kufanya mtihani ambapo wasichana walikuwa 310,248 sawa na asilimia 54.21 na wavulana 262,111 sawa na asilimia 45.79.

Dkt. Mohamed alifafanua kuwa ubora wa ufaulu kwa kuangalia madaraja waliyopata watahiniwa wa shule unaonesha kuwa jumla ya watahiniwa waliopata ufaulu mzuri wa Madaraja ya I - III ni 197,426 sawa na asilimia 37.42 wakati Mwaka 2022 watahiniwa

waliopata ufaulu wa madaraja I – III walikuwa 192,348 sawa na asilimia 36.95. Hivyo, ubora wa ufaulu umeongezeka kwa asilimia 0.46 ikilinganishwa na mwaka 2022.

Ongezekeo hilo la ufaulu wa wanafunzi linatokana na kazi nzuri inayofanywa na walimu katika kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu kama ilivyokusudiwa. Ukiachilia mbali, Kidato cha Nne matokeo ya Darasa la Nne, la saba na Kidato cha Pili yanaonesha ufaulu wa wanafunzi unazidi kuongezeka, na hii ni ishara ya kazi nzuri inayofanywa na walimu.

Tunawapongeza walimu kwa kazi kubwa wanayoifanya. Wito wetu kwa jamii ni kuendelea kuwatia moyo walimu na kuwapatia mazingira mazuri ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Paulina M. Nkwama

Wajumbe

Richard L. Odongo
Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya

Mhariri Mkuu

Gerard J. Chami

Mhariri

Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa

Lucas G. Ogunde

KATUNI



Wasiliana nasi kwa Simu: +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, **S.L.P 353, DODOMA.**



**OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)**

27 JAN.

**Kheri ya Siku
ya Kuzaliwa**

**RAIS WA JAMHURI YA
MUUNGANO WA TANZANIA,
MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN**



www.tsc.go.tz



Tume Utumishi wa Walimu Tanzania

SHULE YA SEKONDARI YENYE MIUNDOMBINU YA KISASA KUZINDULIWA HIVI KARIBUNI

Na Mwandishi Wetu – Dodoma.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, ameridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa Shule ya Sekondari Dodoma City inayojengwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia maarufu kama Shule ya Mfano, Jijini Dodoma.

Akizungumza hivi karibuni mara baada ya kukagua ujenzi huo, Prof. Mkenda amesema kwa hatua ya ujenzi iliyofikiwa Wizara yake iko tayari kufanya uzinduzi kabla ya kuikabidhi shule hiyo Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Mhe. Mkenda alisisitiza kuwa uendeshaji wa shule hiyo unapaswa kuzingatia Sera na Mitaala Mipya ambapo ametaka kuwekwa msisitizo katika Masomo ya Sayansi na kuzingatia uwepo wa Mafunzo ya Amali.

Prof. Mkenda alimpongeza Mkandarasi wa Mradi huo (SUMA JKT) kwa kufanya kazi nzuri na kwa ubunifu, na hasa kutengeneza mfumo wa maji taka utakaowezesha kuzalisha gesi kwa kutoa maji kwa ajili ya



umwagiliaji ambapo hatua hiyo itasaidia kupunguza gharama za uendeshaji wa Shule.

Naye Mkurugenzi wa SUMA JKT, Kanali Petro Mgata, aliahidi kukamilisha shughuli zote zilizosalia ndani ya kipindi cha mwezi mmoja na kukabidhi Shule hiyo tayari kwa uzinduzi na kuanza matumizi.

Kwa upande wake Meya wa Manispaa ya Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe, alisema uwepo wa Miundombinu ya viwango vinavyotakiwa katika Shule hiyo ya Mfano ni kielelezo tosha kuonesha utashi wa Serikali katika kuendelea kuimarisha

miundombinu na kutoa Elimu Bora kwa watoto wa Kitanzania, ili waweze kuchangia Maendeleo ya Taifa lao na Jamii.

“Shule hii ni kivutio cha kujivunia hapa Dodoma na pia ni kielelezo dhahiri cha utashi wa Serikali ya Awamu ya Sita katika kujenga miundombinu bora ya Elimu.” Alibainisha Prof. Mwamfupe.

Shule hiyo ya Mfano inajengwa na Serikali ambapo ikikamilika itakuwa na uwezo wa kupokea Wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja na tayari imeanza kupokea Wanafunzi wa Kidato cha Tano ikiwa na miundombinu yote stahiki.



MCHENGERWA AELEKEZA MSAWAZO WA WALIMU MASHULENI

**Na. Mwandishi Wetu –
Dar Es Salaam.**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikaliza Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Mohamed Mchengerwa, amemuelekeza Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI anayeshughulikia Elimu, Dkt. Charles Msonde, kuhakikisha wanafanya msawazo wa Walimu katika Shule zote zilizopo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Waziri Mchengerwa ametoa agizo hilo mara baada ya ziara yake ya kukagua mapokezi ya wanafunzi wa Kidato cha Kwanza katika Shule ya Sekondari Benjamin Mkapa Jijini Dar es Salaam hibvi karibuni.

Alisema kupitia utaratibu wa viongozi kupita shuleni kupokea wanafunzi wa awali, darasa la kwanza na kidato cha kwanza imebainika kuwepo kwa mlundikano wa Walimu kwenye baadhi ya shule huku kukiwa na Walimu wachache kwenye shule nyingine.

"Sasa namuelekeza Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu OR - TAMISEMI kufanya Msawazo wa Walimu nchi nzima ili kuwe na uwiano sawa wa Walimu na Wanafunzi katika Shule zote. Sio shule ina Wanafunzi wachache lakini ina Walimu wengi ili hali shule zingine zikiwa na Walimu wachache na kuwa na Wanafunzi wengi." Alisema Mhe. Mchengerwa.

"Kila Mtanzania ana haki ya kupata elimu kutoka kwa Walimu waliopangwa na Serikali. Hivyo mgawanyo stahiki ufanyike ili Walimu waliolundikana kwenye shule za mijini wapelekwe kwenye

shule za pembezoni ambazo nazo zina uhitaji mkubwa wa Walimu." Aliongeza Mhe. Waziri.

Akizungumza katika ziara hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mhe. Albert Chalamila alisema hivi karibu alitembelea Shule ya Sekondari Osterbay, Shule ya Msingi Muhimbili na Umoja wa Mataifa na kukuta zaidi ya nusu ya wanafunzi wamesharipoti kwa siku ya kwanza.

"Katika Shule ya Sekondari Osterbay nimekuta ina Wanafunzi takribani 1,000 lakini kuna Walimu 20 tu ilihali katika shule hii ya Sekondari ya Benjamin Mkapa ina Wanafunzi 1,600 na ina

Walimu 100." Alisema Mkuu huyo wa Mkoa.

Mwaka 2024 Idadi ya Wanafunzi waliotegemewa kuandikishwa katika Elimu ya Awali ni 1,877,484 na mpaka Januari 5 mwaka huu Wanafunzi walioandikishwa ni 918,205 sawa na asilimia 48.9.

Kwa upande wa Darasa la Kwanza Wanafunzi walioandikishwa ni 1,191,627 sawa na asilimia 68.9 ya watoto 1,729,180 wenye umri wa miaka saba (7) wanaotarajiwa kusajiliwa.

Pia Wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza kwa mwaka 2024 ni 1,092,960.



MAAFISA ELIMU WATAKIWA KUHAKIKISHA MIRADI YA ELIMU INAKAMILIKA KWA WAKATI

Na. Asila Twaha, OR - TAMISEMI

Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Bw. Adolf Ndunguru amewataka Maafisa Elimu wa Mikoa na Halmashauri kuhakikisha wanafuatilia miradi ya elimu na kukamilisha ifikapo tarehe Januari 15, 2024.

Katibu Mkuu Ndunguru amesema hayo leo tarehe 4 Januari, 2024 wakati akifungua kikao kazi cha Makatibu Tawala Wasaidizi Elimu na Maafisa Elimu wa Halmashauri Kilichofanyika Manispaa ya Morogoro.

Amesema mwaka 2020/21 hadi 2023/24 Serikali imetoa fedha jumla ya shilingi trilion 1.41 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule za awali, msingi na sekondari. Aidha, amesema fedha hizo ziliwezesha kujenga shule mpya 380, vyumba vya madarasa 8,964, mabweni 48, matundu ya vyoo 25,688, nyumba za walimu 857, ujenzi wa mabwalo 6 na ukarabati wa shule na vituo vya walimu 396 kwa elimu ya awali na msingi.

Na kwa upande wa elimu ya sekondari amesema, zimejengwa shule mpya 460, vyumba vya madarasa 13,990, mabweni 1,135, maktaba 4, maabara 295 na mabwalo 103.

Amesema pamoja na jitihada na dhamira njema ya Serikali katika kutekeleza miradi ya elimu lakini bado hajaridhishwa na baadhi ya watendaji ambao wanashindwa kusimamia na

kukamilisha utekelezaji wa baadhi ya miradi kwa muda uliopangwa akitolea mfano kwa baadhi ya mikoa ambayo ujenzi wa miundombinu ya shule bado upo chini ya asilimia 50 licha ya maelelekezo ya Serikali yaliyoelekeza ujenzi ukamilike kabla ya tarehe 30 Disemba, 2023.

“Viongozi wa Mikoa na Halmashauri ambazo ujenzi wa miundombinu ya shule haijakamilika mnatakiwa kujitafakari sana” amesisitiza Nduguru

Katika hatua nyingine Katibu Mkuu Nduguru amewataka maafisa hao kusimamia kikamilifu ufundishaji na ujifunzaji shuleni na kuhakikisha walimu wasiotimiza wajibu wao wanachukuliwa hatua stahiki, huku akiwataka kila Afisa elimu wa Mkoa na

Halmashauri ahakikishe kuwa wanafunzi wote wa darasa la III na kidato cha kwanza wanamudu stadi za lugha ya kiingereza ifikapo mwisho wa mwaka 2024, kuhakikisha wanashirikiana na wadau wengine kuwa wanafunzi wote wa darasa la I na darasa II wanamudu stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu ifikapo mwisho wa mwaka.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais -TAMISEMI anayeshughulikia elimu Dkt. Charles Msonde amewataka maafisa hao kutambua nafasi walizonazo kwa kufanya kazi kwa bidii na waledi na kushirikiana na kutoa wito wahakikishe wanawahudumia walimu kwa upendo, kuwasaidia, kuwasikiliza na kutatua changamoto zinazowakabili na kuwatia moyo akisisitiza kwa kufanya hivyo itafanya kila mtu kufanya kazi zake kwa ufanisi na kutoa matokeo chanya ambayo ndiyo lengo la Serikali la kuwahudumia wananchi wake.



NDEJEMBI AAGIZA UCHUNGUZI FEDHA ZA UJENZI SHULE YA WASICHANA MBEYA



Na. Mwandishi Wetu – Mbeya.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Deogratius Ndejembu, amemuagiza Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo Ndg. Adolf Nduguru, kupeleka Timu ya Wakaguzi kukagua Matumizi ya Fedha kwenye Ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Mkoa wa Mbeya ambayo ujenzi wake unasuasua.

Mhe. Ndejembu ametoa agizo hilo kwenye ziara yake ya kukagua ujenzi wa shule hiyo inayogharimu Shilingi Bilioni Tatu ambayo inajengwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela Mkoani Mbeya.

“Hapa hamjatendea haki fedha hizi zilizoletwa na Mhe. Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa ajili ya watoto wa kike wa Mkoa wa Mbeya. Fedha hizi zilipokuja ni kama fedha zingine za shule na ilitakiwa baada ya kuingia tu mzihamishie kwenye Akaunti ya Shule na siyo kubaki nazo kwenye Akaunti ya Halmashauri ili kuepuka changamoto za mifumo ambazo Wataalamu wenu wanajaribu kuzieleza.” Alisema Mhe. Ndejembu.

“Mngeweza kuhamishia fedha hizi kwenye akaunti hata ya shule jirani kama wenzenu sehemu nyingine walivyofanya na leo msingekuwa mnaongelea

changamoto ya mifumo lakini nyie mkaamua kuzihodhi fedha hizi. Sasa namuelekeza Katibu Mkuu - TAMISEMI kutuma Timu ya Wakaguzi kuja kuchunguza ujenzi wa shule hii ili tuweze kuchukua hatua stahiki haraka.” Alisema Mhe. Ndejembu.

Aidha, alimtaka Mhandisi wa Mradi huo kusimamia masharti ya mkataba wa ujenzi huo kwa kuhakikisha mkandarasi aliyepo analeta idadi ya mafundi wanaotakiwa kuwepo eneo la ujenzi Kisheria na kukamilisha haraka mradi huo ili Wanafunzi wa Kike wa Mchepuo wa Sayansi wa Mkoa huo waweze kunufaika na matunda ya Serikali yao.

CHANGAMOTO ISIWE KISINGIZIO KATIKA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YENU – DKT. MSONDE

**Na. Mwandishi Wetu –
Morogoro.**

Serikali imewataka Watendaji wa Sekta ya Elimu nchini kuacha visingiziowanapotekeleza majukumu yao bali watumie changamoto hizo kama fursa ya kuwaletea Wananchi maendeleo na kuisaidia Serikali.

Kauli hiyo ya Serikali imetolewa hivi karibuni na Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde, wakati akifungua Kikao Kazi cha Nusu Mwaka cha Watekelezaji wa Mradi wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (GPE LANES II) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kilichofanyika katika Manispaa ya Morogoro.

Dkt. Msonde alisema kwa mtendaji yeyote changamoto lazima zitokee katika utekelezaji wa majukumu yake na hapo ndipo

anatakiwa kuzitatua kwa wakati kwani fedha za miradi alizopewa zinatakiwa kutumika kwa wakati ili kutatua changamoto za kielimu zinazoikabili jamii.

“Tuhakikishe kila mtu kwenye eneo lake anatimiza wajibu wake. Simamieni vile mlivyopewa lakini ni lazima mshauri vizuri ili kitu kitokee.” Alisisitiza Dkt. Msonde.

Katika hatua nyingine Dkt. Msonde alisema Mradi wa GPE LANES II umefanya kazi kubwa kwa kushirikiana na Serikali na hivyo watendaji wanapaswa kuhakikisha fedha zote za miradi zimetumika ipaswavyo na kwa muda uliopangwa katika utekelezaji wa miradi hiyo.

“Ni vizuri kuhakikisha kwamba fedha hizi zinapotolewa na Serikali ambazo ni masharti waliyokubaliana na Benki ya Dunia unatekeleza na kukamilisha miradi kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa. Fedha hizi zina deadline (ukomo wa matumizi). Haitakubalika na haikubaliki fedha

yoyote ikafika mwisho wa tarehe ya utekelezaji na haijatumika wakati imeshatolewa.” Alisisitiza Dkt. Msonde.

Kwa upande wake Michael Ligola ambaye alikua Mwenyekiti wa Kikao Kazi hicho ambaye pia ni Afisa Elimu wa Mkoa wa Songwe alisema kikao kazi hicho kina lengo la kufanya tathmini ya utekelezaji wa kazi zilizotekelezwa chini ya Programu ya GPE LANES II kwenye elimu ambapo baadhi ya Halmashauri na Taasisi zimefanya vizuri ijapokuwa taasisi chache zilipata changamoto ya utekelezaji wa miradi.

Akitoa neno la shukrani Adam Shimatayo alimshukuru Mgeni Rasmi kwa kuwatia moyo wa kuendelea kufanya kazi pamoja na kutokuwa na hofu ya changamoto za elimu bali wazione kama fursa na kuzifanyia kazi kwa wakati ili kuliendeleza Taifa.

Mradi wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (GPE LANES II) ulianza mwaka 2019/2020 na unapaswa kukamilika ifikapo Januari 15, 2024 ikiwa ni Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Mradi mwingine mpya wa GPE Multiplier unatarajiwa kuanza.





**OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)**

Jedwali No. 1: Ufaulu wa Jumia Kimadaraja

Daraja	Mwaka	Wawiliana		Wawachana		Jumla	
		Idadi	%	Idadi	%	Idadi	%
A	2022	31,551	4.30	26,779	3.43	58,330	5.45
	2023	21,990	2.95	20,219	2.62	42,209	2.72
	2023	105,557	14.10	113,508	13.85	219,065	14.04
B	2022	102,860	13.87	102,134	12.71	204,994	13.27
	2023	245,670	32.34	244,434	34.73	490,104	33.57
	2023	264,369	36.37	297,528	37.06	561,897	36.36
A-C	2022	305,904	30.60	427,819	52.12	733,723	51.43
	2023	265,659	32.53	473,681	53.23	739,340	52.38
	2023	270,109	32.43	498,629	52.54	768,738	51.52
D	2022	214,347	24.25	241,214	23.55	455,561	30.97
	2023	626,152	81.03	634,547	84.76	1,260,699	82.85
	2023	646,079	81.76	647,050	84.76	1,293,129	83.24
A-D	2022	148,406	18.37	124,629	15.34	273,035	17.05
	2023	135,142	18.22	122,654	15.21	257,796	16.66

Darasa la Nne

Jedwali No. 1: Ufaulu wa Jumia Kimadaraja

Daraja	Mwaka	Wawiliana		Wawachana		Jumla	
		Idadi	%	Idadi	%	Idadi	%
A	2022	28,071	4.39	22,129	3.12	50,200	3.72
	2023	30,292	4.81	23,851	3.26	54,143	3.98
	2023	163,420	25.54	139,509	19.73	302,929	22.47
B	2022	164,636	25.12	150,216	20.65	314,852	23.24
	2023	323,080	50.49	287,187	39.09	610,267	45.43
	2023	317,968	49.50	281,515	38.65	599,483	44.41
A-C	2022	514,577	80.41	558,325	78.01	1,072,902	79.62
	2023	507,820	80.39	585,040	80.68	1,092,860	80.58
	2023	120,363	18.81	145,529	20.55	265,892	19.72
D	2022	118,959	18.86	138,349	19.05	257,308	18.95
	2023	4,963	0.75	3,817	0.54	8,780	0.65
	2023	3,474	0.55	2,854	0.37	6,328	0.45

Darasa la Saba

Jedwali No. 4: Ufaulu wa Jumia Kimadaraja

Daraja	Mwaka	Wawiliana		Wawachana		Jumla	
		Idadi	%	Idadi	%	Idadi	%
I	2022	27,932	9.57	19,933	5.84	47,865	7.56
	2023	55,369	15.48	24,821	6.86	80,190	10.37
	2023	25,843	8.78	19,843	5.76	45,686	7.15
II	2022	39,269	9.32	22,695	6.01	61,964	7.66
	2023	40,620	13.91	33,739	9.88	74,359	11.74
	2023	44,140	13.87	36,310	10.18	80,450	11.67
III	2022	64,315	17.25	73,315	21.47	137,630	20.44
	2023	108,898	33.67	85,775	23.78	194,673	27.73
	2023	161,889	55.42	210,226	61.57	372,115	58.74
IV	2022	190,934	53.95	208,174	60.87	399,108	57.58
	2023	258,104	87.67	283,401	83.05	541,505	80.18
	2023	277,792	87.38	314,869	83.86	592,661	85.31
V	2022	36,011	12.33	57,881	18.95	93,892	14.82
	2023	40,488	12.79	41,530	12.54	82,018	12.66

Kidato cha Pili

Jedwali No. 1: Ufaulu wa Jumia Kimadaraja kwa Wataalamu wa Shule

Daraja	Mwaka	Wawiliana		Wawachana		Jumla	
		Idadi	%	Idadi	%	Idadi	%
I	2022	22,258	9.54	16,690	6.42	37,757	7.29
	2023	24,717	10.54	17,731	6.25	42,448	8.99
	2023	37,484	16.54	30,555	10.94	68,039	13.07
II	2022	28,804	16.34	21,451	11.08	50,255	13.81
	2023	45,728	18.90	40,644	14.62	86,372	16.63
	2023	43,647	17.99	36,876	14.05	80,523	15.87
I-III	2022	105,292	43.64	87,664	31.18	192,956	36.95
	2023	168,368	64.47	149,858	53.37	318,226	57.42
	2023	108,440	44.98	106,187	38.51	214,627	40.94
IV	2022	112,312	46.34	161,080	56.74	273,392	51.94
	2023	213,690	88.60	243,285	87.08	456,975	87.79
	2023	221,286	90.81	256,147	90.11	477,433	90.36
I-IV	2022	27,702	11.40	36,091	12.92	63,793	12.21
	2023	22,385	9.10	33,764	11.89	56,149	10.84

Kidato cha Nne

Salamu za Pongezi Kwa Walimu kwa Matokeo Mazuri ya Darasa la Nne, Saba, Kidato cha Pili, Nne na Sita 2023

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) inawapongeza Walimu, Viongozi wote wa Elimu kwa ngazi mbalimbali na Wanafunzi wa Darasa la Nne, Saba, Kidato cha Pili, Nne na Sita 2023 kwa Matokeo mazuri.

Kila moja wetu aendelee kuongeza jitihada za kiutendaji na Usimamizi mwaka huu 2024 ili kujiandaa mapema kuwa na ufundishaji uliotukuka na hatimaye Wanafunzi wetu waweze kujikomboa kifikra na kuleta maendeleo ya mtu moja na Taifa kwa ujumla.

“

Ni dhahiri kuwa matokeo haya ni kielelezo na dalili nzuri kuwa mwelekeo chanya wa utoaji elimu katika nchi yetu, tunawatakia utendaji wenye tija na kuleta ufanisi zaidi.

#Kazi lendelee



www.tsc.go.tz



Tume Utumishi wa Walimu Tanzania

NDEJEMBI AKERWA NA KASI NDOGO YA UJENZI WA SHULE YA WASICHANA IRINGA

**Na. Mwandishi Wetu –
Kilolo, Iringa.**

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Deogratius Ndejemb, amemuagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo kuhakikisha anamsimamia Mhandisi wa Ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Iringa inayojengwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo kuongeza idadi ya mafundi kama ilivyoelekezwa kwenye Mkataba na ujenzi ufanyike usiku na mchana ili kukamilisha mradi huo kwa wakati

uliopangwa.

Akizungumza wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa shule hiyo, Mhe. Ndejemb ameeleza kutoridhishwa na kasi ya ujenzi huo kutokana na idadi ndogo ya mafundi huku akiagiza kufungwa kwa taa ili ujenzi wa shule hiyo ufanyike usiku na mchana na kukamilika haraka ili Wanafunzi wa Mkoa wa Iringa waweze kunufaika na shule hiyo kama ilivyo dhamira ya Mhe. Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

“Mkurugenzi na timu yako ya Mhandisi na Afisa Manunuzi na Ugavi hakikisheni mnambana Fundi Mkuu wa mradi huu ili aongeze idadi ya mafundi kama

Mkataba unavyosema. Mkataba unasema kila jengo liwena mafundi nane lakini hapa tumekagua tumeona jengo moja lina fundi mmoja hadi wawili, hii haikubaliki na ilitakiwa ikamilike mapema ili ifikapo Januari 8, 2024 Wanafunzi waingie darasani.” Alisema Mhe. Ndejemb.

“Mhe. Rais Samia ameleta fedha Shilingi Biloni Nane kwa ajili ya ujenzi huu. Niwaagize msimamie haraka mafundi waongezwe na ujenzi ufanyike usiku na mchana nataka tuone kasi ya ujenzi huu kwa sababu hakuna chochote kinachokwamisha.” Alisema Mhe. Ndejemb.



KAMATI YA BUNGE YAIPONGEZA TAMISEMI KWA USIMAMIZI WA MIRADI YA MAENDELEO YA ELIMU

Na. Mwandishi Wetu – Iringa.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imeipongeza Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa kusimamia kikamilifu miradi ya maendeleo ya elimu nchini inayotekelezwa katika Halmashauri mbalimbali hapa nchini.

Hayo yamesemwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. Denis Londo, kwenye ziara ya kamati hiyo wakati ikikagua miradi ya maendeleo ya elimu na

miundombinu inayotekelezwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, Wilaya ya Iringa na Mufindi Mkoani Iringa.

Mhe.Londo alisema Kamati imeridhishwa na ujenzi wa miundombinu ya elimu na kupongeza Ofisi hiyo kwa kazi kubwa ya kusimamia na kutekeleza miradi hiyo.

“Rai yangu kwa wataalamu wetu nchini kote ni kuhakikisha wanatumia taaluma zao katika kushauri kwenye kila mradi ambao unatekelezwa na Serikali. Watendaji wetu ndio mnapaswa kuwa wa kwanza kuyaona mapungufu na kuyarekebisha na

siyo kusubiri ije Kamati ya Bunge ama Viongozi wa Kitaifa ndio waje kuona mapungufu.” Alisema.

Naye, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Deogratius Ndejembu, aliishukuru kamati hiyo kwa kutembelea na kukagua miradi hiyo huku akiahidi kuchukua maelekezo yote yaliyotolewa ili kuboresha zaidi katika miradi mingine inayotekelezwa na Serikali kupitia TAMISEMI.

Kamati hiyo inaendelea na ukaguzi wa miradi iliyopo chini ya TAMISEMI katika Mkoa wa Iringa na Mbeya.



NDEJEMBI ASHUHUDIA MAJARIBIO YA MFUMO WA SMART CLASSROOM KUKABILIANA NA UHABA WA WALIMU

Na. Mwandishi Wetu – Pwani & Dodoma.

Naiibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Deogratius Ndejembu ametembelea na kuzindua majaribio ya Mfumo wa Ufundishaji Mubashara “Live Teaching” ambao utawezesha Wanafunzi wa shule nyingine mbalimbali nchini kuunganishwa na Mwalimu anayefundisha katika Shule ya Sekondari Kibaha ili kukabiliana na changamoto ya uhaba walimu nchini.

Akizungumza mara baada ya kujionea majaribio ya mfumo huo ambapo Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Dodoma walikuwa wameunganishwa na Mwalimu anayefundisha kutoka Shule ya Sekondari Kibaha, Mhe. Ndejembu alisema hatua hiyo ni jitihada kubwa ya kukuza elimu inayofanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa pamoja na mipango mingine Mfumo huo ni moja ya mipango ya Serikali katika kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika ufundishaji ili kutatua changamoto ya Upungufu wa Walimu.

“Niwapongeze sana Shirika la Elimu Kibaha kwa kuja na mfumo huo ambao unasimamiwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Hizi zote ni jitihada kubwa zinazofanywa na Rais wetu Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kiwango cha elimu kinakua kwa kukabiliana na changamoto hii ya uhaba wa walimu nchini.” Alisema Mhe. Ndejembu.

Aidha, Naibu Waziri huyo alitoa rai kwa Uongozi wa Shirika

la Elimu Kibaha na Shule ya Sekondari Kibaha kuhakikisha mfumo huo unafanya kazi kama ilivyokusudiwa na Wanafunzi lengwa nchini wananufaika na matunda hayo makubwa yanayofanywa na Rais wao.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, anayeshughulikia Elimu, Dkt. Charles Msonde, alisema wamepokea maelekezo yote yaliyotolewa na Naibu Waziri Ndejembu na kwamba watahakikisha mfumo huo unasambaa kwa kasi nchini ili kila shule iweze kunufaika nao.

Naye, Mkurugenzi wa Huduma za Elimu kutoka Shirika la Elimu Kibaha, Dkt. Rodgers Shemwelekwa, alisema, “Kwa kiasi kikubwa sana mfumo huo utaenda kuondoa changamoto ya uhaba wa walimu kwahiyoyale maeneo yenye uhaba wa walimu sasa wanafunzi wake watakuwa wanaunganishwa na wenzao watakaokuwa wanafundishwa kutokea Shule ya Sekondari Kibaha.”

Uzinduzi wa majaribio hayo ulihudhuriwa na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Franklin Rwezimula ambaye alisema kupitia Kampuni ya Edutech ya China ilitoa seti tatu za vifaa kuwezesha Smart classrooms.

“Vifaa hivyo vimetolewa kwa Taasisi ya Elimu Tanzania ambapo vitatumika kutoa mafunzo kwa Walimu kazini, Shirika la Elimu Kibaha pamoja na Zanzibar.” Alisema Dkt. Rwezimula.

Majaribio hayo yalifanyika kupitia vifaa vilivyotolewa kwa Shirika la Elimu Kibaha ambapo Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Dodoma waliunganishwa na Mwalimu aliyekuwa akifundisha akiwa katika Shule ya Sekondari Kibaha.

Baada ya majaribio hayo kufanyika kutoka Shule ya Sekondari Kibaha kwenda Shule ya Sekondari Dodoma, ilielezwa kuwa mfumo huo utaenda katika shule 10 nyingine na baadaye utasambazwa katika shule zote nchini.





NDEJEMBI ATAKA KIGOMA WAJIELEZE KWA KUTOKAMILISHA UJENZI WA SHULE

Na. Mwandishi Wetu – Kigoma.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Deogratius Ndejembu amemuagiza Afisa Elimu Sekondari wa Mkoa wa Kigoma na Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma kutoa maelezo ya maandishi kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Ndg. Adolf Nduguru ya kwanini walitoa taarifa ya kukamilika kwa Ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Nkungwe ilihali ikiwa bado haijakamilika.

Mhe. Ndejembu ametoa agizo hilo wakati wa ziara yake ya kukagua ujenzi wa Shule za Sekondari katika Wilaya ya Kigoma ambapo ameeleza kutoridhishwa na ujenzi wa shule hiyo huku akimtaka Mkurugenzi

wa Halmashauri kumchukulia pia hatua za kinidhamu Mhandisi wa Halmashauri na Mhandisi anaesimamia mradi huo.

“Namuagiza Katibu Mkuu - TAMISEMI, kwanza apokee maelezo ya maandishi kutoka kwa Maafisa Elimu hawa ya kwanini wametoa taarifa ambazo siyo sahihi. Taarifa walizozileta kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI ni kwamba shule hii imekamilika jambo ambalo siyo kweli.” Alisema Mhe. Ndejembu.

“Tumekagua ujenzi huu wote na tumejionea kwamba madarasa yenyewe bado hayajakamilika, milango haijafungwa, madawati hayajawekwa na hata vyoo vyenyewe bado havijakamilika. Sasa kwa uzembe huu hatuwezi kukaa kimya lazima tuchukue hatua za kinidhamu kwa wote waliohusika.” Alisema Mhe.

Ndejembu.

Alisema Ofisi ya Rais - TAMISEMI haitomvumilia mtu yeyote atakayejarihu kurudisha nyuma jitihada za Mhe. Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye amepokea zaidi ya Shilingi Milioni 600 kwa ajili ya kumaliza changamoto ya Wanafunzi kutembea umbali mrefu.

“Mkurugenzi wa Halmashauri nikuagize pia uwachukulie hatua Watumishi wote ambao wamepewa dhamana ya kusimamia ujenzi huu ikiwemo Mhandisi wa Mradi huu kwa kushindwa kuwajibika ipasavyo kiasi cha kuisababishia hasara Serikali lakini pia kurudisha nyuma maendeleo ambayo Mhe. Rais, Dkt Samia Suluhu Hassan, amepambana kuyaleta Kigoma.” Alisema Naibu Waziri huyo.





OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

Salamu za Pongezi Kwa Walimu kwa Matokeo Mazuri ya Darasa la Nne, Saba, Kidato cha Pili, Nne na Sita 2023

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) inawapongeza Walimu, Viongozi wote wa Elimu kwa ngazi mbalimbali na Wanafunzi wa Darasa la Nne, Saba, Kidato cha Pili, Nne na Sita 2023 kwa Matokeo mazuri.

Kila moja wetu aendelee kuongeza jitihada za kiutendaji na Usimamizi mwaka huu 2024 ili kujiandaa mapema kuwa na ufundishaji uliotukuka na hatimaye Wanafunzi wetu waweze kujikomboa kifikra na kuleta maendeleo ya mtu moja na Taifa kwa ujumla.

“

Ni dhahiri kuwa matokeo haya ni kielelezo na dalili nzuri kuwa mwelekeo chanya wa utoaji elimu katika nchi yetu, tunawatakia utendaji wenye tija na kuleta ufanisi zaidi.

#Kazi lendelee

Darasa la Nne




Darasa la Saba



Kidato cha Pili



Kidato cha Nne



www.tsc.go.tz



Tume Utumishi wa Walimu Tanzania

TUNAMAANISHA TUNAPOSEMA TUMEANZA UTEKELEZAJI WA SERA YA ELIMU



Mafunzo yaendelea kituo cha Misole chenye kata ya Lutende, Miswaki, Miyenze na Mmale wilaya ya Uyui mkoani Tabora.

SHULE 96 KUANZA KUTOA ELIMU YA SEKONDARI MKONDO WA AMALI 2024



Na. Mwandishi Wetu – Morogoro.

Naibu Katibu Mkuu kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Franklin Rwezimula, amesema jumla ya Shule 96 za Sekondari Teule zitaanza utekelezaji wa kutoa Masomo ya Amali, ikiwa ni sehemu ya Utekelezaji wa Mitaala Mipya ya Elimu iliyoboreshwa.

Dkt. Rwezimula ametoa kauli hiyo hivi karibuni Mkoani Morogoro wakati akifungua Mafunzo kwa Walimu kutoka Shule Teule 28 za Serikali na 68 zisizo za Serikali ambazo

zitaanza kutoa Elimu ya Sekondari Mkondo wa Amali katika Awamu ya Kwanza.

Dkt. Rwezimula alimshukuru Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwani maono yake yameleta msukumo mkubwa na kupelekea kuwa na Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023.

Katibu Mkuu huyo alilipongeza Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) kwa kukamilisha Kazi ya Ukaguzi wa Shule Teule, Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) kwa kuongoza Maboresho ya Mitaala ya Elimu pamoja na VETA kwa

Kazi ya Kusimamia Maandalizi ya Utekelezaji wa Mitaala ya Elimu ya Amali.

Nae Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Dkt. Aneth Komba, alisema Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini itaendelea kutolewa kwa muda wa miaka minne na imegawanyika katika mikondo miwili: Mkondo wa Elimu ya Jumla na Mkondo wa Elimu ya Amali.

“Mkondo wa Elimu ya Amali umegawanyika katika michepuo ya fani za Kilimo na Ufugaji, Umakenika, Sanaa Bunifu, Michezo, Ufugaji wa Nyuki, Urembo, n. k. Pia Mwanafunzi atasoma masomo ya Hisabati, Elimu ya Biashara, Kingereza, Historia ya Tanzania na Maadili ili kupata Stadi za Msingi katika Mawasiliano, Stadi za Maisha na Uzalendo.” Alisema Dkt. Komba.

Kwa upande wake Katibu Mtendaji wa NACTEVET, Dkt. Adolf Rutayuga, alisema Mitaala inayotolewa imetengenezwa na VETA na kuhakikiwa na NACTVET, hivyo alizishukuru Taasisi hizo kwa kushiriki kikamilifu kukamilisha kazi hizo kwa weledi na ufanisi mkubwa.





PROF. MDOE ASISITIZA WELEDI KATIKA KUSIMAMIA UTEKELEZAJI MITAALA ILIYOBORESHWA



Na. Mwandishi Wetu – Morogoro.

Naibu Katibu Mkuu kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe, ametoa wito kwa Katibu Tawala Wasaidizi wa Elimu na Maafisa Elimu Msingi wa Halmashauri kwenda kusimamia kwa weledi utekelezaji wa mitaala iliyoboreshwa ili iweze kuleta tija kwa mwanafunzi kama ilivyokusudiwa na Serikali.

Prof. Mdoe ametoa wito huo hivi karibuni wakati akifungua Mafunzo kwa Katibu Tawala Wasaidizi wa Elimu pamoja na Maafisa Elimu Msingi wa Wilaya yaliyofanyika katika Ukumbi wa Shule ya Msingi Bernard Bendel Kola B Mkoani Morogoro.

Alisema, kama wasimamizi wa masuala ya Elimu katika ngazi ya Mkoa na Wilaya ni lazima wakasimamie vizuri utekelezaji wa mitaala hiyo iliyoboreshwa kwani tayari Wizara ya Elimu kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) imetoa mafunzo kwa Maafisa Elimu Kata na Wathibiti Uboza wa Elimu nchi nzima.

Alisema, Taasisi ya Elimu

lifikiwe bila changamoto.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Dkt. Aneth Komba, alisema Mafunzo ya Mtaala ulioboreshwa kwa Viongozi hao wa Elimu ngazi ya Mkoa na Wilaya utasaidia kuongeza ufanisi na tija katika maeneo yao ya utendaji.

Aliongeza kuwa, maboresho yaliyofanyika katika mitaala hii ni pamoja na kuongeza maudhui ya kisasa, kuondoa maudhui yaliyopitwa na wakati na kuondoa kujirudiarudia kwa maudhui katika baadhi ya masomo, pili kupunguza wingi wa maudhui katika masomo ili kuwe na uwiano wa muda wa kujifunza na tatu maboresho katika maeneo ya ujifunzaji wa elimu ya Awali na Msingi.

Akitoa neno la shukrani kwa niaba ya Maafisa Elimu Mkoa na Wilaya, Afisa Elimu wa Mkoa wa Songwe, Mwl. Michael Ligola, aliishukuru Serikali inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutoa fedha nyingi katika kuboresha, kuimarisha na kuendeleza Sekta ya Elimu.





UFAULU WA UPIMAJI WA KITAIFA KIDATO CHA NNE, DARASA LA NNE WAONGEZEKA



Na. Mwandishi Wetu – Dar Es Salaam.

Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) hivi karibuni limetangaza Matokeo ya Mtihani wa Upimaji wa Kitaifa kwa Kidato cha Pili, ambapo Jumla ya Wanafunzi 592,741 kati ya 694,769 wamefaulu sawa na asilimia 85.31. Kiwango hicho cha ufaulu kimeongezeka kwa asilimia 0.13 ikilinganishwa na asilimia 85.18 ya Wanafunzi waliofaulu Mtihani huo mwaka jana.

Akitangaza matokeo hayo Katibu Mtendaji wa NECTA, Dkt. Said Mohamed, amesema Jumla ya Wanafunzi 759,799 walisajiliwa kufanya Mtihani huo, wakiwemo Wasichana 405,878 na Wavulana 353,921.

Alisema kati ya Wanafunzi

waliofaulu kuendelea na Kidato cha Tatu; Wasichana ni 314,949 sawa na asilimia 83.66 na Wavulana ni 277,792 sawa na asilimia 87.28.



Kwa upande wa matokea ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne alisema Jumla ya Wanafunzi 1,287,934 kati ya 1,545,330 sawa na asilimia 83.34 wamefaulu kwa kupata madaraja ya A, B, C na D.

Dkt. Mohamed alisema kumekuwa na ongezeko la ufaulu kwa asilimia 0.39 kwa Wanafunzi wanaoendelea na Darasa la Tano ikilinganishwa na mwaka 2022.

Kati ya Wanafunzi hao Wasichana ni 681, 259 sawa na asilimia 84.79 na Wavulana ni 606,675 sawa na asilimia 81.78.

Katibu Mtendaji huyo alibainisha kuwa Baraza la Mitihani limefuta matokeo yote ya Wanafunzi 178 waliofanya udanganyifu na Wanafunzi watatu (3) walioandika lugha isiyo na staha katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne.

Pia Baraza hilo limewafutia matokeo Wanafunzi 28 waliofanya udanganyifu na Wanafunzi 14 walioandika lugha isiyo na staha katika Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili.

WANAFUNZI WANAOMUDU LUGHA YA KIINGEREZA WAONGEZEKA - MCHENGERWA

**Na. Mwandishi Wetu –
Morogoro.**

Viashiria vya Upimaji wa Utendaji Kazi wa Walimu kuanzia Januari hadi Desemba mwaka 2023 vimeonesha kuna ongezeko la Wanafunzi wa Darasa la Kwanza wanaomudu Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kutoka asilimia 35 hadi 94.4.

Hivi karibuni akifunga Kikao Kazi cha Katibu Tawala Wasaidizi wa Elimu na Maafisa Elimu wa Halmashauri kilichofanyika ndani ya Manispaa ya Morogoro, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Mohamed Mchengerwa alisema idadi ya Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza wanaomudu stadi nne za lugha ya Kingereza (Kusikiliza, Kuongea, Kusoma na Kuandika) imeongezeka kutoka asilimia 32

hadhi 82.

Aidha, alisema kwa Darasa la Pili umahiri wa Stadi za KKK umeongezeka kutoka asilimia 77.9 hadi 95 huku idadi ya Wanafunzi wa Darasa la Tatu wenye uwezo wa kujitambulisha na kuelezea mazingira yao kwa lugha ya kingereza umeongezeka kutoka asilimia 35 hadi kufikia asilimia 77 mwezi Desemba 2023.

Waziri Mchengerwa alisema kuongezeka kwa uwezo huo wa Wanafunzi waliomaliza Elimu ya Msingi Mwaka, 2023 kutoka asilimia 79.82 kwa mwaka 2022 hadi asilimia 80.58 mwaka 2023 ni mafanikio chanya kwa Jamii na Taifa na hiyo inazidi kuonyesha matunda ya jitihada za Serikali katika kuimarisha ujifunzaji na ufundishaji nchini.

“Wanafunzi wa Sekondari wanaopata chakula cha mchana shuleni wameongezeka kutoka

asilimia 50.41 hadi kufikia asilimia 62.69 Desemba, 2023. Na katika kipindi hicho, Wanafunzi wa Shule za Msingi wanaopata chakula shuleni wameongezeka kutoka asilimia 50 hadi kufikia asilimia 66.4.” Alisema Waziri Mchengerwa.

“Nitumie fursahi kuwapongeza kwa dhati Walimu wote wa Shule za Msingi na Sekondari nchini pamoja na Wasimamizi wa Elimu katika ngazi za Kata, Halmashauri, Mikoa na Taifa kwa kazi kubwa na nzuri mnayoifanya katika kuhakikisha Wanafunzi wanapata ujuzi, maarifa na stadi.” Alisema Mhe. Mchengerwa.

Aliwapongeza Wakuu wa Mikoa, Katibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Viongozi wa Kisiasa wote kwa jitihada, utashi wao na ushirikiano wanaowapa Walimu katika kutekeleza majukumu yao.



WALIMU NDIO ELIMU, TUWASIKILIZE ILI KUZIJUA CHANGAMOTO ZAO - DKT. MTAHABWA



Na. Mwandishi Wetu – Morogoro.

Kamishna wa Elimu Tanzania, Dkt. Lyabwene Mtahabwa, ametoa wito kwa Wathibiti Ubora wa Shule na Maafisa Elimu Kata kuwaheshimu Walimu na kuwasikiliza ili kufahamu changamoto zao hali itakayosaidia kuboresha Sekta ya Elimu nchini.

Dkt. Mtahabwa ametoa wito huo hivi karibuni Mkoani Morogoro wakati akifungua Mafunzo ya Mtaala ulioboreshwa kwa Wathibiti Ubora wa Shule na Maafisa Elimu Kata, mtaala ulioanza kutekelezwa mapema Januari, 2024.

“Elimu katika nchi yoyote ile ni Mwalimu. Ukijua hilo jifunze kufanya kazi vizuri na Mwalimu, jifunze kumheshimu Mwalimu, kumpenda, kumthamini tusitoe maelekezo bila kuwapa elimu ya jambo lolote. Naomba tutumie nafasi zetu vizuri na kuingea nao kwa staha.” Alisema

Aliongeza kuwa, Sera ya Elimu ya Mwaka 2014, Toleo la Mwaka 2023, inasisitiza kuinua hadhi ya elimu, hivyo alitoa wito kwa wataalamu hao kuwa wanyenyekevu kwa Walimu

wanaowaongoza na kuacha tabia ya ujuaji wa kila kitu, hali itakayosaidia kuleta matokeo chanya katika Sekta ya Elimu nchini.

Kwa upande wake Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Msingi na Elimu ya Awali kutoka OR – TAMISEMI, Bi. Suzanne Nusu, alisemakama Watekelezaji wa Sera katika ngazi ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa watahakikisha wanatoa ushirikiano kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Taasisi ya Elimu Tanzania ili Mtaala

huo ulioboreshwa uende kuwa chachu ya mabadiliko katika Sekta ya Elimu.

Nae, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Dkt. Aneth Komba, alitoa wito kwa Wathibiti Ubora wa Shule kuzingatia kwa undani mafunzo hayo yanayotolewa na TET ili kwenda kuwafundisha Walimu wote kwenye Kata zao kuuelewa Mtaala Mpya na namna bora ya kuutekeleza.

Alisema, Maafisa Elimu Kata na Wathibiti Ubora wa Shule ni wawakilishi wa TET katika maeneo yao ya utendaji hivyo ni muhimu kusaidia kutatua changamoto zinazowakumba Walimu katika shule zao badala ya kuandika taarifa ya changamoto hizo bila kusaidia utatuzi.

Dkt. Komba alisema, Taasisi ya Elimu Tanzania itaendelea kushirikiana na Maafisa Elimu Kata pamoja na Wathibiti Ubora wa Shule ili kuhakikisha Ubora wa Elimu unatekelezwa katika ngazi zote ikiwemo kupitia mitaala iliyoboreshwa.





WANAFUNZI WOTE WALIOANDIKISHWA NA KUFAULU WAANZE MASOMO JANUARI, 2024

**Na. Mwandishi Wetu –
Dar Es Salaam.**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Mohamed Mchengerwa, amewaagiza Wakuu wa Mikoa kutekeleza maagizo mbalimbali ili mchakato wa kuwapokea Wanafunzi Wapya katika Shule za Awali, Msingi na Sekondari uende kwa ufanisi.

Mhe. Mchengerwa, ametoa agizo hilo hivi karibuni wakati akizungumza na Wakuu wa Mikoa katika Kikao Kazi kilichofanyika kwa njia ya mtandao ambapo viongozi hao walieleza hatua zilizofikiwa katika Miradi ya Elimu na walivyojipanga kuwapokea Wanafunzi wapya.

Hata hivyo, Wakuu wa Mikoa hao kwa nyakati tofauti wakiwasilisha maelezo yao kuhusu utekelezaji wa miradi ya elimu walimhakikishia Waziri Mchengerwa kuwa hakuna Mwanafunzi atakayekaa chini

au kukosa darasa na kuwa wote walioandikishwa na kufaulu wataanza masomo kwa wakati mmoja.

Aidha, Waziri Mchengerwa aliwaagiza Wakuu wa Mikoa ambao bado hawajakamilisha Ujenzi wa Miundombinu mbalimbali ya Elimu kuhakikisha wanakamilisha baadhi ya majengo ya vyumba vya madarasa ifikapo Januari 15 kama walivyoahidi wakati wanatoa Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Elimu katika mikoa yao.

"Mimi na Wasaidizi wangu tutapita kila Mkoa, Halmashauri na Wilaya kukagua miradi mbalimbali ya elimu kama ambavyo mlimeweka ahadi za utekelezaji," Alisema.

Maagizo mengine aliyoyatoa ni pamoja na shule zote mpya zinazojengwa zisajiliwe hususan zile za Wasichana na baada ya mchakato huo kukamilika zianze kazi mara moja ya kupokea Wanafunzi.

Alisema baadhi ya mikoa ukiwamo wa Mkoa wa Pwani

wameanza mchakato huo na kuna mikoa wamekamilisha ujenzi wa shule mpya kati ya asilimia 75 hadi 80, lakini bado shule hizo hazijasajiliwa wala kupokea Wanafunzi, kama maelekezo ya Waziri Mchengerwan yalivyowataka Wakuu wa Mikoa kusajili shule zote.

"Naomba msimamie usajili na mapokezi ya Wanafunzi wanaojiunga na Elimu ya Awali, Darasa la Kwanza na Kidato cha Kwanza. Hakikisheni Wanafunzi wanasajiliwa bila masharti." Alisema Mhe. Mchengerwa.

Pamoja na hayo Waziri huyo aliwataka Wakuu wa Mikoa kusimamia vema Bajeti ya Chakula kwa Wanafunzi katika Shule zote za Bweni ili kuhakikisha wanapata chakula hicho kama inavyotakiwa na katika ubora na viwango vinavyostahili.

Mhe. Mchengerwa alisema kwa kuwa Januari mwaka 2024, Serikali imeanza kutekeleza Mtaala Mpya wa Darasa la Kwanza na Darasa la Tatu, Wakuu wote wa Mikoa wanatakiwa kusimamia maelekezo yaliyoainishwa katika Sera Mpya ya Elimu.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Ndg. Albert Chalamila, alisema katika Mradi wa kuimarisha Elimu ya Sekondari walipokea kiasi cha Shilingi Bilioni 13.0 kwa ajili ya Ujenzi wa Shule za Sekondari 15 kati ya hizo 13 zimekamilika huku zingine zikiendelea kukamilishwa.

"Tulipokea pia Shule 15 za Msingi kati ya hizo Shule 13 zimekamilika, katika taarifa yetu Dar Es Salaam, kuna shule nne (4) ambazo hazijakamilika. Lakini Mkoa wa Dar Es Salaam una changamoto ya ardhi, ndio maana kuna shule tunajenga shule kwa mfumo wa maghorofa." Alisema Chalamila.



WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA YAENDELEA NA KAZI YA KUWANOA WALIMU KUHUSU MTAALA MPYA WA ELIMU



Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yaendelea na kazi ya kuwanoa Walimu kuhusu Mtaala Mpya wa Elimu, ambapo jumla ya Walimu 620 kutoka Kata zote 20 za Halmashauri ya Wilaya ya Monduli walishiriki mafunzo hayo yaliyofanyika hivi karibuni.

WATOTO WOTE WALIOTOKA NJE YA MFUMO RASMI WA ELIMU KWA SABABU ZOZOTE ZILE WANARUDI SHULE - PROF. MKENDA

Na. Mwandishi Wetu – Dodoma.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, ameiambia Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuwa Serikali itaendelea kuhakikisha watoto wote waliotoka nje ya mfumo rasmi wa elimu kwa sababu zozote zile wanarudi shule ili kupata elimu na ujuzi na kutimiza ndoto zao za kuwaletea

maendeleo binafsi naya Taifa.

Prof. Mkenda aliongeza kuwa Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) wanatarajia kufanya tathmini ya kwanza ya watoto waliokatisha masomo kwa sababu mbalimbali na kisha kurudi shuleni baada ya Serikali kutoa Waraka wa kuwarudisha ili kuona kama wana changamoto zozote na jinsi ya kuboresha mafunzo yao.

“Tumekubaliana na UNICEF tufanye programu ya kwanza

kwa kushirikiana ya kutathmini Wanafunzi waliorudi shuleni baada ya Tangazo la Serikali, tutakaa na kuongea nao kuangalia changamoto zilizopo na kuzitafutia ufumbuzi.” Alisema Waziri huyo.

Aliongeza kuwa kuna programu mbalimbali za mafunzo kwa watoto na vijana walio katika masomo kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDC), Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima na wengine wamerudi katika mfumo rasmi.

WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA YAENDELEA NA KAZI YA KUWANOA WALIMU KUHUSU MTAALA MPYA WA ELIMU



ZINGATIENI MAFUNZO KUEPUSHA SERIKALI KUCHUKIWA NA KUINGIA GHARAMA ZA KISHERIA - KATIBU MKUU IKULU



Na. Mwandishi Wetu – Mwanza.

Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – Ikulu, Ndg. Mululi Mahendeka, hivi karibuni amefungua Mafunzo ya Uzingatiaji Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma kwa Makatibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Makatibu Tawala Wasaidizi, Wataalamu wa Utawala na Rasilimali Watu na Wanasheria wa Serikali kutoka katika maeneo tofauti ya Utumishi wa Umma hapa nchi na kuwataka kuzingatia mafunzo hayo ili kuwepo na tija katika utoaji huduma kwa Watumishi na Wananchi.

Katibu Mkuu Mahendeka alisema kutokana na kutoeleweka kwa Miongozo ya Sheria hiyo imechangia kuwepo kwa mlolongo wa malalamiko kutoka kwa Watumishi na Wananchi ambayo yanawafikia viongozi wa juu hivyo kuchangia kuzorotesha utendaji kazi wa Taifa kwa ujumla.

“Ndugu washiriki wa mafunzo haya ambao wengi wenu ni Watumishi wenzangu, Ofisi ya Rais imeingia gharama ya kuandaa mafunzo haya kwa siku tano ikitambua umuhimu wake. Mkizingatia ipasavyo Sheria, Kanuni na Taratibu mtaiepusha Serikali kuchukiwa na kuingia gharama zinazotokana na mashauri yanayotokana na

wahusika mliopewa dhamana ya kusimamia maeneo yenu kushindwa kuwajibika kikamilifu.” Alisema Katibu Mkuu Ikulu.

Alibainisha kuwa hakuna sababu ya kuwapa kazi Viongozi wa Juu akiwemo Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Madini au Katibu Mkuu Kiongozi ya kutatua kero za Wananchi na Watumishi wakati waliopewa jukumu hilo wapo lakini wameshindwa kutimiza wajibu wao.

“Kushindwa kutafsiri vizuri Sheria, Kanuni na Taratibu imechangia Watumishi kutumia muda mwingi kwenye Vyombo

vya Kisheria kusaka haki yao na kushinda mashauri yao na mwishowe Serikali kuingia gharama.” Aliongeza Ndg. Xaveri Daud, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mwenyeji wa mafunzo hayo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza, Ndg. Balandya Elikana, aliishukuru Ofisi ya Rais kwa kufanyia mafunzo hayo Mkoani humo na kuwataka washiriki wote kuja na matokeo chanya baada ya kuelimishwa vyema.

“Tunapotoa huduma bora kwa Wananchi na Watumishi, imani kutoka kwao inazidi kuongezeka kwa Serikali yao hali itakayokuwa na tija katika utendaji wao wa kazi na majukumu yao ya kila siku kwa ujumla.” Alisema Katibu Tawala huyo.

Washiriki wengine katika mafunzo hayo walitoka kwenye Taasisi za Serikali, Wataalamu wa Sheria na Rasilimali Watu kutoka Mikoa ya Shinyanga, Mara, Geita, Simiyu, Mara, Kagera na Mwanza.

Pia Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina M. Nkwama alialikwa na kushiriki mafunzo hayo akiwa ameambatana na Mkurugenzi wa Utawala na Menejimenti ya Rasilimali Watu, Ndg. Zachary Dida.



ZINGATIENI MAFUNZO KUEPUSHA SERIKALI KUCHUKIWA NA KUINGIA GHARAMA ZA KISHERIA - KATIBU MKUU IKULU





MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

 Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania

 [tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)